Shule za Msingi na Fedha

Je, Serikali inasemaje kuhusu ada na michango?

Kwa mujibu wa Mkakati wa Kuondoa Umaskini (PRS) na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (PEDP), Serikali imefuta michango yote ya lazima kwa shule za msingi tangu Januari 2002. Hii ina maana kwamba hakuna mtoto atakayezuiwa kuhudhuria shule kwa sababu ya kushindwa kulipa michango. Shule au uongozi wa kijiji hawaruhusiwi kumlazimisha mtu yeyote kulipa fedha kwa elimu ya msingi kwa ajili ya karo, madawati, ujenzi, vitabu, vya kiada, gharama za mikutano, au kwa ajili ya shughuli nyingine yoyote. Serikali imefanya hivyo ili kuhakikisha kwamba watoto wote, pamoja na walio masikini, wanapata elimu ya msingi.

Hata hivyo, wazazi na wanajamii, wanahimizwa kushiriki kikamilifu na kuchangia kwa kadri ya uwezo wao. Kilicho muhimu hapa ni kwamba mchango wowote ni lazima uwe wa hiari. Kwa mfano, jamii inaweza kujitolea nguvukazi yenye kuhitajika katika ujenzi wa nyumba za walimu, vyoo na nyenzo za maji. Wanaweza pia kuwasaidia walimu kwenye shughuli za mitaala ya ziada.

Je, fedha zitatoka wapi sasa?

Wazazi, walezi na wanajamii wataendelea kuwajibika katika kutoa chakula, mavazi, malazi, mapenzi na matunzo kwa watoto wao. Wanatakiwa pia kuwa na ari ya kufuatilia yale ambayo kila mtoto anafanya awapo shuleni, na kuwasaidia katika juhudi zao.

Serikali inadhamiria kuongeza fedha kwa ajili ya shule za msingi. Ongezeko la hivi karibuni la makusanyo ya kodi, lina maana kwamba kuna rasilimali zaidi kwa ajili ya elimu kutoka kwa walipa kodi. Wafadhili wetu pia wamekubali kuongeza fedha. Fedha za Serikali na za wafadhili zinatakiwa kuwekwa pamoja badala ya kutumiwa katika miradi mbalimbali inayoendeshwa na wafadhili tofauti. Sehemu kubwa ya fedha hizi zitatumwa kwenye shule na halmashauri za mitaa.

Kuna fedha nyingine tena zinazotumwa katika ngazi ya jamii?


Kuna fedha nyingine aina tatu zinazotumwa katika ngazi ya jamii kwa ajili ya elimu ya msingi:

- Ruzuku kwa ajili ya kujenga uwezo: (Capacity Building Grant): Hizi ni fedha kwa ajili ya kuimarisha uwezo na nguvu za watendaji katika ngazi ya jamii, kata na wilaya ili kutekeleza MMEM. Umuhimu wa kipekee utawekwa katika kujenga uwezo wa kamati za shule, ambazo kulingana na MMEM zinatakiwa kupokea Dola 500 za Marekani (Takribani sh. 500,000/=) kwa mwaka kwa ajili ya lengo hilo.

- Ujira wa Utumishi: (Personnel Emoluments): Hizi ni fedha kwa ajili ya mishahara ya walimu. Kulingana na maelekezo ya Rais, walimu wanatakiwa kulipwa kwa wakati. Mishahara inatakiwa kutumwa si zaidi ya tarehe 25 ya kila mwezi.

- Gharama Nyinginezo: (Other Charges): Hizi ni fedha zinazotumwa kwa shughuli nyingine





ambazo si za mishahara. Zinatumwa kwenye Halmashauri za Wilaya na zinatakiwa kutumika kwa ajili ya elimu ya msingi. Sehemu kubwa ya fedha hizi zinatakiwa kunufaisha shule. Kiasi kitumwacho kinatofautiana katika kila wilaya. Lakini kinachapishwa katika magazeti kila baada ya miezi mitatu na Wizara ya Fedha. Maofisa wa ngazi za wilaya wanatakiwa kubandika matangazo katika sehemu za wazi ili kila mwananchi aone ni kiasi gani cha fedha kimetumwa kwao.

Je, uwajibikaji unafanyika vipi?

Ili kuboresha maendeleo ya shule na kuhakikisha fedha zinatumika vizuri, kila shule inahitajika kutengeneza mpango wa shule na bajeti. Mpango unatakiwa kutengenezwa na kusimamiwa na kamati ya shule kwa kushauriana na walimu, wanafunzi, na wanajamii wengine.

Kipengele kimoja muhimu sana katika MMEM ni uwazi na uwajibikaji. Kamati za shule zinatakiwa kutoa ripoti kwa viongozi wa kata na wilaya, lakini pia kwa jamii. Mipango na bajeti zinatakiwa kuwa wazi kwa kila raia. Taarifa kuhusu fedha zilizopokelewa na jinsi zilivyotumika zinatakiwa kubandikwa hadharani na kuwekwa wazi kwa watu wote, wakiwemo wazazi na wanafunzi. Katika hotuba yake ya Septemba 2002 juu ya MMEM, Rais Mkapa alizungumzia suala hili kwa msisitizo:

> "Ili kuimarisha demokrasia, kila shule inawajibika kutoa taarifa ya mapato na matumizi kwa serikali ya kijiji au mtaa kila baada ya miezi mitatu katika Mkutano wa Serikali ya Kijiji au Mtaa. Sambamba na kutoa taarifa katika vikao mbalimbali, Halmashauri na shule wanawajibika kutoa matangazo kuhusu fedha zilizopokelewa, na matumizi yake, katika mbao za matangazo za Halmashauri, shule na sehemu za mikusanyiko ya wananchi. Lazima sasa kila mwananchi ajue ni kiasi gani cha fedha kimepokelewa katika Halmashauri au shule yake, na jinsi zilivyotumika....Huo ndio uwazi, uwajibikaji na utawala bora tunaoutaka..."

Nitafuatiliaje?

Kila mtu ana haki ya kupata habari, na kila mmoja ana haki ya kufahamu juu ya fedha za MMEM. Kwa kuwa sasa unafahamu juu ya haya mambo, unaweza kuangalia kama yanafanyika katika jamii yako, uliza maswali kama hayafanyiki na utoe mchango wako wa mawazo yenye kujenga ya kufanya mambo yawe bora zaidi. Kwa mfano, unaweza kufuatilia na kuona kama taarifa ya fedha za shule inawekwa katika mbao za matangazo. Unaweza kuuliza kama fungu kamili la fedha za ruzuku kwa kila mwanafunzi zimepokelewa na kama zinatumika vizuri. Jadili taarifa hizi na wengine. Una haki ya kuuliza maswali na kupata majibu fasaha. Kwa mujibu wa mabadiliko ya Serikali, haikubaliki tena kwa kiongozi kutoa amri tu bila kuwasikiliza watu. Ni dhahiri mabadiliko huchukua muda, na hatutegemei kwamba kila kitu kitakuwa timilifu mara moja. Hata hivyo, una haki ya kuona maendeleo yakitokea.

Unaweza kupata habari kutoka kwa mwalimu mkuu, Afisa Elimu wa Wilaya, Diwani au Mbunge wako. Unaweza kuomba taarifa kutoka Mkutano wa Kijiji/Mtaa au vikao vya Halmashauri. Unaweza pia kuuliza Asasi Zisizo za Serikali (AZISE) katika eneo lako.

hakielimu

SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (022) 2151852 / 3 • Faksi (022) 2152449 • info@ hakielimu.org • www.hakielimu.org